*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo


## Kimbunga Chido chaua 45 Msumbiji



**MAPUTO, Msumbiji**

IDADI ya vifo vilivyotokana na kimbunga Chido nchini Msumbiji, imeongezeka na kufikia watu 45.

Idadi hiyo imetolewa na Taasisi ya Kitaifa ya Kudhibiti Majanga nchini humo.

Takwimu za awali zilizotolewa juzi zilionesha kuwa kimbunga hicho kilisababisha vifo vya watu 34 baada ya kuupiga Mkoa wa Kaskazini wa Cabo Delgado Jumapili iliyopita.



## Wanajeshi 100 wa Korea Kaskazini wauawa, 1,000 hoi

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

TAKRIBAN wanajeshi 100 wa Korea Kaskazini wameuawa katika mapigano katika vita vya Ukraine tangu waingie kwenye mapigano upande wa Urusi mapema mwezi huu, Mbunge wa Korea Kusini amesema.

Lee Sung-kwon, akizungumza na waandishi wa habari baada ya Bunge kupewa taarifa na Idara ya Kitaifa ya Ujasusi ya nchi hiyo, alisema wengine 1,000 wamejeruhiwa.



## 'Syria sasa si tishio tena kwa majirani

**DAMASCUS, Syria**

KIONGOZI wa serikali isiyo rasmi wa Syria, Ahmed al-Sharaa, amesema nchi hiyo imechoshwa na vita na si tishio kwa majirani zake wala kwa nchi za Magharibi.

Katika mahojiano na BBC mjini Damascus, al-Sharaa ametaka vikwazo dhidi ya Syria viondolewe.

"Sasa, baada ya yote yaliyotokea, vikwazo lazima viondolewe kwa sababu vililengwa kwa utawala wa zamani.


| ISSN 2953-2787 | Bei Tanzania Sh. 1,000 | Ijumaa Desemba 20, 2024 |


# AWAMU HII KIBOKO!

# 'Wazungu wa unga' hawapenyi

## ●Kilo 614.12 zateketezwa Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, imeteketeza kilo 614.12 za dawa za kulevya katika Kiwanda cha Saruji cha Twiga jijini Dar es Salaam.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, alisema kati ya dawa zilizoteketezwa, kilo 601.87 ni methamphetamine na kilo 12.25 ni heroin.

Kamshina Jenrali Lyimo alifafanua kuwa dawa hizo zilikuwa zinashikiliwa kielelezo ambapo Mahakama za Hakimu Mkazi Kisutu na Kibaha, ziliamuru uteketezaji wake kutokana na hatari ya kuharibika au kubadilika umbo wakati kesi husika bado zinaendelea.

Alifafanua kuwa uteketezaji wa dawa hizo unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya mwaka 2015 na kanuni zake. Sheria hii inaruhusu uteketezaji wa dawa hizo kufanyika kabla, wakati au baada ya shauri kumalizika mahakamani.

Aidha, Kamshna Jenerali Lyimo alisema uteketezaji huo unafanywa kwa njia zinazozingatia usalama wa afya za watu na utunzaji wa mazingira na kusimamiwa na wadau mbalimbali waliotajwa kisheria.

Wakati huo huo, Kamishna Jenrali Lyimoamesema kwa mwezi huu wa Desemba peke yake, mamlaka imeteketeza ekari 12 za mashamba ya bangi mkoani Tabora na kilo 398.105 za dawa mbalimbali mkoani Mtwara na kwamba siku chache zijazo, Mamlaka inatarajia kuteketeza kilo 126.21 za mirungi mkoani Arusha.



## Balozi Dk. Nchimbi atua Tabora ziara ya siku mbili

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, yuko mkoani Tabora kwa ziara ya siku mbili. Mara baada ya kuwasili juzi Uwanja wa Ndege wa Tabora, alipokelewa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Said Juma Nkumba na viongozi wengine wa Chama.

Aidha, alipokea taarifa ya utendaji wa kazi wa Chama kutoka kwa Katibu wa CCM Mkoa wa Tabora, Wilson Nkhambaku na taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paulo Matiko Chacha.



## Waziri Masauni: Tumepiga hatua usimamizi na uhifadhi mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Hamad Masauni amesema Serikali imepiga hatua katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira licha ya changamoto zinazojitokeza.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye ziara ya kikazi Zanzibar na kuongeza kuwa ushirikiano wa viongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais umeleta tija katika sekta ya mazingira.

"Nina siku chache tangu nimeingia katika wizara hii, lakini najiona mtu mwenye bahati kwani kwa muda mfupi tangu nimekuja, nimejifunza vitu vingi kama nimekaa miaka miwili na hii inatokana na kuwepo kwa timu nzuri kwani ni watu wenye kasi katika utendaji wao wa kazi," alisema.


rifaly

Habarika kidijitali! Soma gazeti la Uelekeo ndani ya Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com